



## Mwenye kutakiwa kheri na Allah, (Allah) humuonja kutokana na kheri hiyo

Imepokewa Kutoka kwa Abuu Huraira -Radhi za Allah ziwe juu yake- amesema:  
Amesema Mtume -Rehema na amani ziwe juu yake-: "Mwenye kutakiwa kheri na Allah,  
(Allah) humuonja kutokana na kheri hiyo.

[Sahihi] [Imepokelewa na Al-Bukhaariy]

Anaeleza Mtume -Rehama na amani ziwe juu yake- yakuwa Mwenyezi Mungu akitaka kheri kwa yeyote katika waja wake waumini huwapa mtihani katika nafsi zao na mali zao, na familia zao, kwa kile kinachotokea kwa muumini ikiwemo kurejea kwa Allah Mtukufu kwa maombi na dua, na kufutiwa makosa, na kunyanyuliwa daraja.

<https://sunnah.global/hadeeth/sw/show/4204>

